

KIZIDUO:

MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARULA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KUJADILI HOJA ZA MKAGUZI WA NDANI ROBO YA KWANZA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KILICHOFANYIKA TAREHE 22.10.2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA

A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA

1. Mhe. Yanga E. Makaga	M/kiti – H/W	Mwenyekiti
2. Mhe. Makoye L. Sengerema	M/Kiti Kamati ya Kudhibiti UKIMWI	Mjumbe
3. Mhe. Fortunatus Nzwagi	M/Kiti Kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira	“
4. Mhe. Enock S. Ndekeja	M/Kiti Kamati ya Maadili	“
5. Mhe. Mathias H.Mashauri	M/Kiti Kamati ya Elimu,Afya na Maji	“
6. Mhe. Betty Dacman	Diwani Viti Maalum	“
7. Mhe. Modesta L. Bulugu	Diwani Viti Maalum	“
8. Mhe. Tryphone S. Male	Diwani Kata ya Kasenyi	“
9. Mhe. Mbugai Majumba	Diwani Kata ya Mission	“
10. Ndg. Ally Salim Ally	Kaimu Mkurugenzi Mtendaji(W)	Katibu

B: WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

1. Mhe. Tabasamu H. Mwangao Mbunge

C: WATAALAM WALIOHUDHURIA

1. Dr.Saumu Kumbisaga Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
2. Ndg. Alex Tabaro Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi
3. Ndg. Dorothy Haki Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
4. Ndg. Ghati D. Matiko Kny Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
5. Ndg.Christopher Mpogole Kny Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi
6. Ndg. Prosper Luasha Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
7. Ndg. Ashura Kajuna Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi
8. Ndg. Edgar Heri Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA

D: MWANDISHI WA VIKAO

1. Ndg. Evance Mwankenja Paul
2. Ndg. Magreth M.Paul
3. Ndg. Fidelis S. Elias

Muht.Na.1/10/2021 – Kufungua kikao

Katibu: Aliwakaribisha wajumbe katika kikao ambapo aliwaeleza kwamba pamoja na kwamba kikao hicho kimeitishwa mahususi kwa ajili ya kujadili taarifa ya mkaguzi wa ndani robo ya kwanza mwaka wa fedha 2021/2022 lakini pia watajadili taarifa zingine ambazo ni muhimu kwa wajumbe kuzipitia na kutolea maamuzi ambayo ni ya muhimu kwa ustawi wa Halmashauri na wananchi kwa ujumla. Kisha alimkaribisha mwenyekiti ili aweze kufungua kikao.

Mwenyekiti: alianza kwa kusoma sala ya Halmashauri na kisha aliwasihi wajumbe kujielekeza katika kujadili taarifa zitakazo wasilishwa na kwamba kila mmoja atangulize maslahi ya wananchi kwanza. Kisha alifungua kikao mnamo saa 7:30 mchana.

Muht.Na.02/10/2021 – Kuthibitisha agenda za kikao

Wajumbe walithibitisha agenda za kikao zifuatazo

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda za kikao
3. Taarifa ya uthamini na ulipaji wa fidia eneo la stendi ya Bukala
4. Taarifa ya redio Sengerema
5. Taarifa ya mkaguzi wa ndani robo ya kwanza
6. Taarifa ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Halmashauri ya wilaya ya Sengerema
7. Taarifa ya Mapokezi ya fedha Tsh. 2,780,000,000/= kupitia fedha za Uviko -19
8. Kufunga kikao

Muht.7/10/2021 – Taarifa ya Mapokezi ya fedha Tsh 2,780,000,000/= ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 129 kupitia fedha za Uviko -19


Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji(W): Aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha kutoka serikali kuu kiasi cha Tsh2,780,000,000/= kwa mchanganuo ufuatao:- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 129 kwa shule za sekondari Tsh. 2,580,000,000/= , Ujenzi wa bwani la Watoto wenye mahitaji maalum Tsh. 80,000,000/= na Ujenzi wa madarasa 6 katika shule shikizi 3 Tsh. 120,000,000/=. Hivyo utekelezaji wa miradi hii umeshaanza na kamati mbalimbali za ujenzi zimeshaundwa na hatua zinazoendelea ni ukamilishaji wa upatika naji wa mafundi na hatua za manunuzi wa vifaa unaendelea.

Wajumbe waliipokea taarifa na walishauri kwamba mchakato wa manunuzi uharakishwe ili kuwezesha kukamilisha kwa ujenzi wa madarasa hayo kwa muda uliotolewa na serikali. Kwa hiyo walielekeza menejimenti kujipanga kikamilifu kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ubora na kwa kuzingatia taratibu za manunuzi ili kuepusha hoja za ukaguzi. Kisha walirdihia.

Muht.Na.8/10/2021- Kufunga kikao


Katibu: Aliwashukuru wajumbe na kwamba aliwaeleza kwamba watayatekeleza ushauri wote. Kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga kikao.

Mwenyekiti: Aliwashukuru wajumbe na kwamba alisisitiza kuwa yale yote yaliyoazimiwa Menejimenti ihakikishe inayatekeleza. Kisha lifunga kikao saa 10:18 jioni...



Yanga E. Makaga

MWENYEKITI



Binuru M. Shekidele

KATIBU

UMETHIBTISHWA LEO TAREHE 17.11.2021